KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 9, Issue 3

11th Jumâ al-Awwal 1432

15th April, 2011

YALIYOMO

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU NI 'IBADA? 1 - 4

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU NI IBADA?

Mtayarishi: Daarul Watan

Kila sifa njema zinamthubutukia Allâh, ambaye amejitosheleza, na Rehma na Amani ziwe juu ya Mtume mwenye kuchaguliwa na mjumbe mwenye kuteuliwa na yeyote mwenye kufuata nyenendo zake na kushikamana nazo. bâda ya hayo;

Hakika ya ndoa ni neema kubwa ya Allâh (سبحانه وتعالى) juu ya waja wake, nayo ni njia ya mapenzi, na njia ya mafanikio, na anuani ya utulivu, nayo ni dalili miongoni mwa dalili za Allâh (سبحانه وتعالى) inayojulisha Utukufu wake. Allâh (سبحانه وتعالى) amesema: **"Na miongoni mwa dalili zake kwamba hapana shaka amewaumbia nyinyi kutokana na nafsi zenu wake ili mupumbae nao. Na akatia kati yenu mapenzi na kite (huruma). Hapana shaka katika hayo, ni mazingatio kwa watu wanaozingatia".** [Surat ar-Rum:21]

Nao ni mwito wa fikra ambayo Allâh amewaumba watu juu yake, na Sunnah miongoni mwa Sunnah za Mitume wa Allâh, na njia ya kisheria iliyo halali inayohukumu maingiliano na uondoaji wa matamanio. Pia ni kifungo cha kuwazuia vijana wa kiume na wa kike kutokana na fitina na upotofu, na ni njia rahisi na nyepesi kwa ajili ya kujichumia malipo na thawabu kutoka kwa Allâh mtukufu, bila ya tabu wala uzito wowote na ni njia ya kupatikana umma wingi wa Ki-Islamu na kuzidisha nguvu zake na kuwapata vijana wa kiislamu wenye nguvu na kuwaogopesha mâdui wa Uislamu. Na ni mlango unaotimiza kujuana baina ya Waislamu yakaenea mapenzi juu yao na mafungamano.

Kuwepo kwa ndoa husababisha nafsi kupata ladha na utulivu, na kusimamishwa kwake huanzisha mipangilio ya maisha haya kuhifadhika. Vilevile hufanya mambo yakanyooka, kukapatikana kutosheka kwa uhakika, na pia kukapatikana watoto na kusalimika mujtama' mzima kutokana na maradhi.

Kwa ajili ya mambo yote hayo na mengine mengi ametuwekea sheria Mola wetu kuowana na akatuhimiza juu yake na kututia hamu ndani yake, na akaturahisishia njia zake, Allâh akasema katika Surat an-Nur aya 32: **"Na waozeni wajane miongoni mwenu (waungwana"** na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema katika hadeeth ambayo ni swaheeh ambayo wameafikiana Al-Bukhâri na Muslim kuwahimiza vijana juu ya kuoa: *"Enyi Mabarobaro! Mwenye kuweza kuoa miongoni mwenu, basi na aowe, kwani kufanya hivyo, macho yatainamishika, tupu zitahifadhika, na yule ambaye hawezi, basi juu yake ni kufunga, kwani huko kufunga ni kinga"*.

Hapana shaka hakika ya ndoa ni yenye furaha na mapambo, na nafsi hupenda jambo linaloingiza furaha ndani yake, kwa ajili hiyo, umeweka mipaka Uislamu na adabu kwa ujumla na nyenendo za kisheria jinsi ambavyo tunafurahi na kusherehekea,

Kwa vile ni hakika ya Muislamu kusherehekea na kufurahi pindi anapopata neema au akawa na amani ya uhakika ndani ya dini yake na dunia yake kwa mfano kuoa, basi furaha yake hii itabidi kumtukuza na kumshukuru Mwenye kumneemesha ambaye si mwengine asiyekuwa Allâh Mtukufu, kwani laiti si yeye asingaliipata furaha hiyo, au ikamhalalikia kushereheka, na Shukrani inatakikana kwa Mwenye kushukuru kuiambatanisha furaha yake na mâmbatano ya kisheria, na wala asiifanye neema hii njia ya kutumbwikia katika yale aliyoyaharamisha Allâh Mtukufu.

Na wala asisahau Muislamu katika kufurahi kwake huku kwamba iko furaha ya uhakika ambayo hakuna furaha kama hiyo bâda yake, na furaha hii ni kufurahi kwa kumtii Allâh na kujibashiria habari njema kwa fadhila zake na Rehma zake kama anavyosema Allâh kaika Surat Yunus aya ya 58 **"Sema kwa fadhila za Allâh na Rehema zake basi kwa hayo wafurahike hayo ni bora kuliko yale wanayoyakusanya."** nayo ni furaha ya nyoyo ambayo huleta shauku, basi mtu akatenda matendo ambayo yatamkurubisha katika miji ya furaha katika mabustani na mito katika makazi ya kikweli mbele ya Mfalme mwenye kukadiria kila kitu, ni furaha ambayo inakuwa katika kufika kumtwi'i Allâh na kujikurubisha kwake, amesema "Ali (رضي الله عنه) "Siku ambayo ndani yake sikumu'asi Allâh basi kwangu hiyo ni Iddi". Ama furaha kwa ajili ya dunia na kupata starehe zake

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU NI IBADA?

zenye kuondoka na kumalizika hapa hapa, hiyo si furaha ya uhakika kama anavyosema Allâh Mtukufu katika Surat ar-Ra'd aya 26 **"Na wanafurahia maisha ya kidunia, na hayakuwa maisha ya duniani katika maisha ya Âkher isipokuwa starehe yenye kupita."**

Muislamu anatakikana maisha yake yote yawe ni kwa ajili ya Allâh (سبحانه وتعالى), asifanye vitendo, wala kusema lolote, wala kuinua hatua yoyote isipokuwa iwe ni kwa miongozo ya kitabu cha Allâh na Sunnah za Mjumbe wake (صلى الله عليه وسلم) kusadikisha neno lake Allâh aliposema katika Surat al-An'âm aya 162: **"Sema hakika swala yangu, na kuchinja kwangu, na maisha yangu, na kufa kwangu, yote ni kwa ajili ya Allâh Mola wa Walimwengu wote."** Basi awe katika hali zake zote amezungukwa ni sheria wala asipinduke mipaka, katika furaha yake na huzuni yake, afurahi kama anavyotaka Allâh kufurahi, wala asitamke ila lile ambalo amemhalalishia Allâh, asifanye kibri wala ku'asi, wala kupotoka kutokana na ukweli, bali aimarishe furaha yake kwa kumkumbuka Mola wake ambaye ametimiza juu yake neema ya kuoa, na akamruzuku kutokana na mazuri, na kumtengezea sababu za kufurahi na kushereheka. Na vile vile anapopata huzuni asitamke yale yanayomchukiza Allâh na kumghadhibisha,wala asisikitike na kukata tamâ kutokana Rehma za Mola wake, na aridhike aliyomkadiria Allâh na kusubiri na awe katika hali zake zote na tabia zake na mambo yake yote ni mwenye kufuata na kutekeleza sheria za Allâh (سبحانه وتعالى)

Kutokana na ukamilifu wa Hikma za Allâh na Rehma zake kwa waja wake hakutuacha bure-bure, bali ametuwekea mipaka vipi tufurahi na vipi tuhuzunike? na wala hakutuacha katika furaha zetu na huzuni zetu, katika sherehe zetu na misiba yetu tufurahi na kuhuzunika tutakavyo, wala hakutuacha kwa ajili ya mila yetu kujifanyia tunavyotaka na kutuchezea sheitani namna itakavyokua.

La kusikitisha ni kwamba watu wengi katika zama zetu hizi imani zao zimedhoofika, ni wachache wa kumcha Allâh, na umezidi ujinga kwenye hukmu za ki-Dini, wakapinga uongofu aliokuja nao Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) katika kusherehekea na kufurahi, zikapambaukiwa furaha zao kujikita kwenye mila na matamanio ya nafsi zao, yakapatikana ndani yake kukhalifu sheria na munkar (uovu) ulio mwingi na makosa kurundukika, na kukosekana kutwi'i na kuondoka kwa barka, hapo tena ndoa hiyo ikawa ni nukhsi (nuhusi) tupu, na mambo yakabadilika bâda ya wema ikawa uovu, na bâda ya mapenzi ikawa machukivu.

Sasa wacha tuonyeshe katika risala hii kwa ujumla zile mila na desturi zilizoenea katika furaha zetu, na yale ambayo yanapingana na sheria ya Mola wetu, na kukhalifu uongofu wa Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم), na lengo letu hapa ni kuwanasihi Waislamu na kuwahadharisha kutokana na mila na yale yenye kukhalifu ili isije ikageuka bâda ya kuwa neema ikatupeleka kwenye mângamivu, na furaha ikawa ni huzuni.

MILA NA DESTURI AMBAZO ZINAPINGANA NA SHERIA KATIKA FURAHA NA MAHARUSI

1) KUCHANGANYIKA WANAUME NA WANAWAKE WA KANDO:

Na sampuli zake ni kama zifuatazo:

Kuingia mume na jamâ zake, na jamâ wa mke - wanaume wakati anawekwa biharusi kwenye kiti ametolewa kumuona na amevishwa nguo zilizo kinyume cha sheria. Vile-vile kuingia wafanyakazi wa ma-hoteli ama ma-holi wakati wa furaha kwenye sehemu walizokâ wanawake, na pia kuingia wapiga picha ama camera kwa wanawake na kuanza kuwapiga na kuweka kwenye DVD ama CD na ma-Albamu, lengo ni kuipamba hafla hiyo, na yasiokuwa hayo kutokana na mchanganyiko wa manaume na wanawake kwenye maharusi. Haya ni masikitiko makubwa na msiba ulio mkubwa, na hapana shaka mchanganyiko wa waume na wake ajnabii ni haramu, na ni njia kubwa mno na nyepesi ya kufanya maovu, kwa hakika ametuhadharisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) mambo hayo katika hadeeth swaheeh ilioafikiwa na al-Bukhâri na Muslimu aliposema: "*Jiepusheni kuingia kwenye wanawake.*" mmoja katika Maswahaba akasema; "Unaonaje kama ni shemegi Ewe Mjumbe wa Allâh? Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Shemegi ni mauti.*" na ufisadi wa kuchanganyika kwa ujumla ni mwingi unaojuilikana, tunamuomba Allâh atusalimu salama.

2) **TABARRUJ:**

Kutoka nje ovyo wanawake, wanatoka kwenda kwenye sherehe huku wamejipamba kwa kikamilifu, na picha ya kutoka ovyo kwenda maharusini na kwengineko kwenye sherehe ni nyingi, nazo ni kuvâ nguo fupi au zenye mapambo yakuvutia yenye kuleta fitina ua nguo za kubana ambazo zinaonyeha uchi na kubagua viungo vyote vya mwili, na kujitanda kwa vitandio vidogo vyenye kurembeshwa, bali wamevuka mipaka wanawake wengi kila namna ya uharibifu wa tabia, na kupuuza kila mila na desturi zilizo njema, wakawa kama mtoto wa bandia kwa huziharibu nyuso zao, wakavâ nguo ambazo haziwasitiri miili yao ila kidogo tu, kupaka dawa nywele zao kuwa njano na nyekundu, kuvâ nguo za sampuli zenye kupasuliwa na kuonyesha nyuchi zao, kutia nywele za bandia, kunyoa nyusi zao, na yasiokuwa hayo yajuilikanayo na yashuhudiwayo kwenye furaha zetu. Wako wapi wanawake aliosema Allâh katika Surat al-Ahzâb aya 59 **"EWE MTUME, WAMBIE WAKE ZAKO NA WATOTO WAKO NA WANAWAKE WA KIISLAMU WAJISTIRI WAJIANGUSHIE VIZURI**

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU NI IBADA?

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

JILBABU ZAO ILI ZIWAFUNIKE NYUSO ZAO NA VICHWA VYAO." na kauli yake Allâh katika Sura hiyo hiyo aya 33: **"NA WALA MSITOKE NJE YA MAJUMBA YENU OVYO BILA YA KUJISTIRI NA KUDHIHIRISHA MAPAMBO KAMA WALIVYOKUWA WAKIFANYA WANAWAKE KABLA YA KUJA UISLAMU."** Hivi wanawake hawaogopi kauli ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: "*MAKUNDI MAWILI NI KATIKA WATU WA MOTONI, SIJAYAONA, (1)NI WATU WENYE MIJELEDI MFANO WA MIKIA YA NG'OMBE WAKAWA WANAPIGIA WATU. (2)NA WANAWAKE WALIOVÂ HALI WAKO UCHI, WENYE KWENDA KWA MARINGO HUKU WAKIANGALIWA, VICHWA VYAO KAMA NUNDU ZA NGAMIA ZINAZOYONGA, HAWATAINGIA PEPONI NA WALA HAWATAPATA HARUFU YAKE NA HARUFU YAKE ITAENEA SEHEMU MBALI MBALI.*" Imepokewa na Muslimu.

3) KUTOKA WANAWAKE MAJUMBANI MWAO HALI NI WENYE KUJIPAMBA NA KUJITIA MANUKATO, NA KUPITA MBELE YA WANAUME:

Jambo ambalo ni haramu kisheria, kaika hadeeth iliyopokewa na Imâm Ahmad na akaipa daraja la uzuri Sheikh al-Albâni Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*MWANAMKE YEYOTE ATAKAYETIA MANUKATO AKAPITA MBELE YA WANAUME WAKAPATA HARUFU YA MANUKATO HAYO BASI YEYE NI MZINIFU.*"

4) KUWEKA MASPIKA MAKUBWA NA VYOMBO VYA MATAARABU AMA MIZIKI NA KUANZA KUCHEZA NA KUJINENGUA VIUNGO VYAO:

Hili bâdhi ya watu wameona ni jambo zuri hata wakawa ni wenye kutoa mualiko wa kadi kualika harusi ya mtoto wa fulani na fulani tutakuwa na muimbaji fulani ama ngoma fulani, upuuzi mwingi kushuhudiwa na nyimbo ambazo zinasaidia kuvunja mâdili, jambo ambalo linaeneza uovu, uchafu, uharibifu na ubadilikaji wa tabia kwa vijana wanaoinukia wakiume na wa kike, na kuacha athari mbaya katika nyoyo. Jambo ambalo hapana shaka ni upuuzi mtupu na haramu, na dalili za uharamu wa hayo ni nyingi, miongoni mwazo ni kauli ya Allâh (سبحانه وتعالى) katika Surat Luqmân aya 6 **"NA WAKO MIONGONI MWA WATU WANUNUAO UPUUZI WA MAZUNGUMZO ILI KUWAPOTEZA WATU KATIKA NJIA YA ALLÂH PASI-KUWA NA ELIMU."** Na upuuzi wa mazungumzo kama alivyosema Ibn Mas'ud na wengineo yakwamba ni nyimbo na Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*KUTAKUWA NA WATU KATI KA UMATI WANGU WATAHALALISHA TUPU, NGUO ZA HARIRI, TEMBO NA MIZIKI.*" Imepokewa na al-Bukhâri.

Ama yasiokuwa hayo kutokana michezo ambayo ndani yake hamuna vivutizi vibaya vya kuleta uharamu inafâ, yenye kukusanya maneno mazuri, tungo za kuwaombea harusi, pia kuwepo kwa dufu wala sio ngoma, na tena sharuti iwe ni wanawake watupu bila ya wanaume, na kusipatikane nyuma yake fitina kama vile kudhihiri sauti za wanaume, na wala kusiwe na mchanganyiko wa waume na wake, na huku ndiko kutangaza ndoa na kutofautisha mambo yanayoleta uharamu.

5) KUPIGA PICHA IWE "*PHOTOGRAPH*" AU VIDEO:

Huu ni munkar (uovu) mkubwa unaopatikana katika sherehe na furaha zetu, ulioleta misiba mikubwa na mizito kwa watu wengi, kwani ni familia ngapi zilikuwa namshikamano na maelewano ya hali ya juu zikavunjikilia mbali kwa sababu ya picha au video? ni wanawake wangapi waliokuwa na heshima zao zikaharibiwa sifa zao na majina yao kwa kupatikana picha zao katika mikono ya wanaume ambao hawamuogopi Allâh (سبحانه وتعالى) ? Pamoja na kuwa picha na video ni uovu bali ni katika madhambi makubwa, na hawakua ila ni wenye kulaaniwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), wapigaji picha. Nao watakuwa ni wenye adhabu kali siku ya qiyama.

6)STAGE KWA AJILI YA MAHARUSI WAWILI:

Ni sehemu ambayo huwekwa juu ya kiti harusi, mbele ya watu, na jambo hili hakika ni munkar na halifai.

Amesema Sheikh 'Abdul Azeez bin Bâz (رحمه الله): "Na katika mambo maovu yaliyozushwa katika zama hizi ni kuweka stage kwa ajili ya maharusi katika kumbi za wanawake, na kuketishwa mume hadharani ya wanawake hawakuvâ mavazi ya sheria wako uchi, na huenda akaingia yule mume na ndugu zake wa kiume, na hapana kuficha juu ya yule mwenye fikra iliyosalimika na wivu wa kidini hayakuwa mambo haya isipokuwa ni ufisadi ulio mkubwa, na yawezekana wanaume ajnabii walioingia sehemu hiyo wakawashuhudia wanawake waliovâ ovyo wakavutika nao yakapatikana mipango yakuingia kwenye mângamivu. Lililo wajibu ni kuzuia mambo hayo kwa kuvunja fitina hizo na kuuchunga mujtamâ wa wanawake na mambo yanayokhalifu sheria zenye kutakasika.

7)VAZI LENYE KUKHALIFU SHERIA:

Huvishwa biharusi **JIGUO** kubwa kupita kiasi, tena jeupe, likaburutika mpaka wapatikane watu wa kulishikilia ili aweze kutembea, bila-hivyo hawezi kutembea, na wengine huvalia soksi nyeupe lakini wengi hawavai soksi hizo ili ionekane piko na hina walizotiwa, hii ni mila mbaya kabisa na mifumo michafu ambayo Mujtamâ wetu umeathirika na makafiri, nako ni kujifananisha nao na mila ambazo hazina asili ndani ya Qur'an tukufu wala Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم), mambo hayo hakuyafanya Mtume (صلى الله عليه وسلم)

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU NI IBADA?

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

wala Maswahaba zake, wala watu wema waliotutangulia. Na kama ndani yake muna kheri, basi wangelitutangulia kufanya hivyo, kwani ndani yake muna isrâf na uharibifu ulio mkubwa kiasi cha kununuliwa **JIGUO** La ghali, tena kubwa kupita kiasi na halivaliwi isipokuwa mara moja tu, Allâh (سبحانه وتعالى) amesema katika Surat al-A'arâf aya 31 **"NA WALA MSIZIDI KIASI (ISRAFU) HAKIKA ALLÂH HAWAPENDI WENYE KUPITA KIASI."**

8) ISRAFU NA UHARIBIFU KATIKA MASHUGHULI YA HARUSI:

Nayo inakuwa hivi:

Kupatikana isrâf katika chakula cha harusi (WALIMA) kupikwa chakula kingi pasina haja ikafikia kubakia na kutupwa na hali yakuwa wako maskini na mafukara wanaokihitaji chakula hicho.

Vile vile kukodisha sehemu za kusimamishia shughuli hiyo ikawa ni mzigo mzito kwa mume akazongwa na madeni ya hali ya juu kiasi cha kumaliza harusi kuanza msingi mpya. Na kuwakodi watumbwizaji tarabu waume na wake au ngoma yoyote hayo ni mambo ambayo ndani yake kunapatikana uharamu.

Mambo yote haya huwapelekea vijana wengi kushindwa kuoa kutokana na kukosa uwezo wa kutosha wa kuyafanya mambo hayo, msiba ambao ni mkubwa.

9) HONEY MOON:

Huandamana mume na mke na kusafiri kabla au bâda ya mwezi, yawezekana kuwa zaidi ya hapo, kuingia miji ya kikafiri, nazo ni mila mbaya na mazingira mabovu yanayofanywa na mujitamâ wa Ki-Islamu, kama watu wamekuwa vipofu hawaoni kwa kuwafuata makafiri. Hapo tena ndani yake ikawa ni ufisadi ulio mkubwa na fitina kubwa na tabia chafu zitakazokuwa kwa mume na mke walizovuna kwenye safari yao. Huathirika mume na mila ya kikafiri na kuwafuata mpaka ikafikia kupuuza dini yake na mila njema za Ki-Islamu, na mke pia akâthirika na ukafiri huo akavua vazi la dini na taji la haya, akapuuza tabia na mila ya Ki-Islamu zilizo njema, na kuwaona wanaofanya hivyo wamepitwa na maendeleo, akageukia kwenye uovu na kuanza kuvâ mavazi ya maajabu ya utupu.

10) KUKESHA MPAKA IKAFIKIA KUCHELEWA KUTOKA KWENYE HAFLA (SHEREHE):

Jambo ambalo linawapelekea kukosa Swala ya alfajiri kwa jama'ah upande wa wanaume, na wanawake kuwapatisha madhara watoto na watu wa nyumba zao na kusababisha kukasirika kwa waume zao. Kesha hii ni haramu kama alivyosema Sheikh 'Abdul 'Azeez bin Bâz:

NENO LA MWISHO:

Nimeona kwa ndugu zangu Waislamu, wanaume na wanawake bâdhi ya mila na mifumo ambayo yanapatikana katika furaha zetu na harusi zetu, ambazo zinapingana na sheria na miongozo ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), nazo zote ni sababu ya kuiga upofu wa watu waliokufuru na kupotea, na sasa nawabainishia jawabu la suali hili:

JEE FURAHA ZETU NI MILA AU IBADA?

Masikitiko makubwa yaliyopo ni kuwa watu zaidi hujiendea kimatamanio kuliko kuendea sheria na dini, na ndipo bâdae tunajiuliza, ni kwa nini migogoro mingi na matatizo ya hali ya juu hupatikana kwa wanandoa na kupatikana talaka nyingi? Kumbe hatukujua sababu ya yote hayo ni kuwa tulianza maisha yetu vibaya kwa kuikhalifu sheria na kupingana na Allâh kwa kufanya na kudhihirisha mâsi, ikwa matokeo yake ni kukosekana raha ya nafsi, maisha mazuri ya ndoa, na utulivu wa kisawa-sawa. Na njia swaheeh ya kupata maisha yaliyo mazuri na yenye utulivu na baraka hapana kujitakasa kwa kuacha mila hii mibaya, na kuiga mifumo batili, na kuendea miongozo itokayo kwenye kitabu cha Allâh na Sunnah za mtume (صلى الله عليه وسلم) sio katika furaha zetu tu bali katika maisha yetu yote. Allâh amesema katika Surat al-Anfâl aya 24 **"ENYI WATU MULIOAMINI ITIKIENI MWITO WA ALLÂH NA MTUME WAKE PINDI WANAPOKUITENI MUAMINI, JUENI KUWA HAPANA SHAKA ALLÂH HUINGIA KATI YA MTU NA MOYO WAKE, NA KWAKE YEYE MTAKUSANYWA."**

Tunamuomba Allâh azifanye siku zetu zote ziwe za furaha, na azitwahirishe nyoyo zetu na unafiki, na mtendo yetu yaepukane na riya', na Rehma na amani ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم).

NENO LA BUSARA

"

Baadhi ya wanafunzi wadogo wa 'ilmu [ya ki-Sheriya] husema kuwaambia wenzao wanaofanana nao [kwa daraja ya 'ilmu]: Msimamo wenu ni upi kumuhusu mtu ambaye fulani bin fulani alimtangaza yakwamba ni mzushi? Itakulazimu ujitokeze msimamo wako bila ya kuchelewa; na lau kama si hivyo basi sisi tutakukata hata wewe!

"

Sheikh 'Abdul-Muhsin al-'Abbaad